

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI

(EWURA)

MALALAMIKO NAMBA. SN.71/135/105

JANETA KONDO MLALAMIKAJI

DHIDI YA

SHIRIKA LA UGAVI WA UMEME NCHINI (TANESCO)..... MLALAMIKIWA

TUZO YA MAKUBALIANO

(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia waraka wake Na. 19 wa tarehe 15 Oktoba, 2021)

1.0 Maelezo ya Awali:

Mnamo tarehe 11 Januari 2021, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bi. Janeta Kondo ("Mlalamikaji") akilalamika dhidi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) (Mlalamikiwa). Mlalamikaji anadai kuwekewa deni linalotokana na ankara ya umeme deni ambalo Mlalamikaji anadai alishalipa kwa awamu nne mwaka 2009 kufuatia makubaliano baina yake na Mlalamikiwa.

Mlalamikaji anaeleza kuwa, ghafla mwaka 2020, Mlalamikiwa alirejesha deni la kiasi cha TZS 1,192,908.10 akimtaka Mlalamikiwa kulipa. Mlalamikaji anadai deni hilo alishalilipa mwaka 2009 kufuatia makubaliano baina yake na

Mlalamikiwa ambapo Mlalamikiji alilipa deni hilo kwa awamu nne. Hatimae Mlalamikaji alileta malalamiko yake EWURA na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kufuta deni hilo ili kumpunguzia adha na usumbufu.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, Mamlaka (EWURA) mnamo tarehe 13 Januari, 2021 ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta utetezi wake ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa kanuni ya 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T.S na. 428/2020 '*Rule 7 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*'.

Mnamo tarehe 25 Januari 2021, Mlalamikiwa alileta utetezi wake akaiieleza Mamlaka kwamba, Mlalamikaji alikuwa anadaiwa kiasi cha TZS 1,472,968.10 ikiwa ni deni la matumizi ya umeme. Mlalamikiwa alidai kuwa Mlalamikaji aliomba kwa Mlalamikiwa aondolewe riba kwenye deni hilo na aweze kulipa jumla ya TZS 1,192,908.10 baada ya kuondolewa riba ya TZS 280,060.00 Mlalamikiwa aliendelea kudai kwamba Mlalamikaji alilipa jumla ya TZS 635,000.00 mpaka tarehe 11/02/2010 hivyo kuvunja makubaliano yaliyofikiwa ya kulipa deni lake bila riba. Mlalamikiwa alisema yupo tayari kurejesha huduma ya umeme kwa Mlalamikaji mara tu atakapolipa deni lake.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande zote mbili kilifanyika tarehe 19 Februari 2021 na tarehe 31/03/2021 katika Ukumbi wa ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki. Katika kikao cha usuluhishi, wadaawa walikubaliana kwamba Mlalamikiwa atafanya hesabu upya ikiwa ni pamoja na kufuta riba yote na kiasi kitakachokokotolewa Mlalamikaji atapaswa kulipa kwa awamu mbili.

Mnamo tarehe 17/08/2021, Mamlaka (EWURA) ilipokea barua kutoka kwa Mlalamikiwa akieleza kuwa wamefikia muafaka kati yake na Mlalamikaji na kwamba Mlalamikaji amelipa deni lake na hakuna madai kati yao. Kikao cha kuhitimisha shauri hili kilifanyika tarehe 09/09/2021 katika ukumbi wa ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki.

Mwishoni, muafaka kati ya Mlalamikaji na Mlalamikiwa ulifikiwa kwa makubaliano kwamba;

- a) Mlalamikiwa alifanya ukokotoaji wa deni kwa kushirikiana na Mlalamikaji na kupata kiwango sahihi cha deni baada ya marekebisho ya kuondoa riba; na
- b) Mlalamikaji amelipa kiasi cha TZS 488,323.55 tarehe 12/08/2021 na kwamba hadaiwi tena na Mlalamikiwa.

Makubaliano yaliyoorodheshwa hapo juu yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye kanuni ya 14(4) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T.S namba 428/2020 na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba:

- i. Mlalamikiwa amefanya ukokotoaji wa deni kwa kushirikiana na Mlalamikaji na kupata kiwango sahihi cha deni baada ya marekebisho ya kuondoa riba; na
- ii. Mlalamikaji amelipa kiashi cha TZS 488,323.55 tarehe 12/08/2021 na kwamba hadaiwi tena na Mlalamikiwa

na kwa mujibu wa kanuni ya 14(5) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Utatuzi wa Migogoro T.S namba 428/2020, makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

IMETOLEWA KWA LAKIRI ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati
na Maji (EWURA) Dodoma tarehe 15 Oktoba, 2021.



.....
KAPWETE LEAH JOHN
KATIBU WA BODI

